# MAOMBI

## SHUKRANI

Namshukuru Yesu kwa kuniwezesha kutoa toleo hili la kwanza la kitabu cha MAOMBI. Kitabu hiki namtolea Yesu na Baba yake mapenzi yake yatimie kwa walioitwa na Yesu kuwa wahubiri. Awanurukishie akili zao zipate uelewa au ufahamu juu ya kusudi lake ktk maisha yao. Asante Baba wa Yesu na Yesu pia. Amen.

**MHUBIRIWA KIMATAIFA MINISTRY, FIRST EDITION 2024**

ISBN: 1986 - 08 - 08 - 01

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki hakiruhusiwi ku-nakili, kutafsiri au kuchapishwa kwa njia yoyote bila ru-husa ya Mhubiri wa Kimataifa ministry au Mhubiri wa Kimataifa Lameck Lister. Nakuu zote zimetoka ktk bib-lia (Maandiko matakatifu in Swahili Union Version)

**MHUBIRI WA KIMATAIFA MINISTRY.**

ADDRESS: S.L.P 9332, DAR ES SALAAM

TANZANIA (EFATHA)

MOBILE: +255658601034

EMAIL: listlameck5@gmail.com

MAOMBI.

1.Maombi ni nini?……………………………………………..

2. Kwa nini uombe?…………………………………………..

3. Aina za maombi……………………………………………

4. Jinsi Kuomba……………………………………………….

5. Maombi yaliyo mapenzi ya mungu………………….

6. Mambo ya kuzingatia kabla kuomba……………….

7. Jinsi kufahamu majibu ya maombi………………….

8.Nani aombe?………………………………………………..

9.Shukrani……………………………………………………..

10.Sala nini?……………………………………………………..

11.Tofauti ya Maombi na Sala…………………………….

12.Roho mtakatifu……………………………………………..

13.Neno La Yesu………………………………………….

14.Kuokoka…………………………………………………….

15. Mwisho…………………………………………………….

# 1. MAOMBI NI NINI?

Ni njia ya kumueleza Mungu haja/mahitaji ya moyo wako. Mahitaji ni yale yaliyoshindikana kwako sio kwa mwingine.Haja au mahitaji ya moyo wako hufamika kama kiu ya moyo wako.Mfano; kiu ya kumwona mungu,haja kuona nguvu za kazi ktk utumishi wake,mahitaji ya moyo wake ya chakula, malazi,pesa,mavazi,watoto, utajiri,Gari n.k

**"1Wathesalonike 5.17 ombeni bila kukoma"**

Maombi ni sehemu ya maisha ya waliokoka , Mahitaji au haja za moyo wako ni mpya mara kwa mara.unahitaji kuomba kila siku na unapoomba jambo mbele Baba wa mbinguni omba kwa bidii bila kukata tamaa.

Ee mtu wa kimataifa uliyeokoka wewe ni kama mtoto change mbele za mungu mwenye mahitaji mbalimbali unahitaji Baba wa Mbinguni aliyekuzaa kwa njia ya Yesu na Roho mtakatifu akuhudumie.Kwa kawaida mababa wa kidunia hufurahi watoto zao wadogo wawaombapo hata kama ya wanayoomba wakati mwingine huona si muhimu bali huwapa.

**Math 7:9—11**

**" Au kuna mtu yupi kwenu, ambaye, mwanawe akimwomba mkate, atampa jiwe?**

**Au akiomba samaki, atampa nyoka? Basi ikiwa ninyi, mlio waovu, mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema, je! Si zaidi sana Baba yenu aliye mbinguni atawapa mema wao wamwombao?"**

Mungu ni mwema jifunze kuomba mema peke yake ndiyo atakayokupa.Mfano Amani, Mavazi,Furaha,Utajiri,hekima,Roho mtakatifu

Rehema kwa ajili ndugu wasamehewe wakosapo waliokoka kama wewe.

## 2.KWA NINI UOMBE

Ee mtu wa kimataifa uliyeokoka zipo sababu za lazima zinazotaka wewe ukae ktk maombi ili umueleze mungu yale unayotaka.Baadhi ya sababu hizo ni kama zifuatazo;

- Uepushwe na majaribu au vishawishi

**Mathayo 26:41**

**“Kesheni, mwombe, msije mkaingia majaribuni; roho i radhi, lakini mwili ni dhaifu. “**

- Ni njia ya ushirika na Mungu.Maombi hukupa haki ya kuwasiliana Mungu kama Yesu na kusikilizwa.

**Marko 6:46**

**“Hata alipokwisha kuagana nao akaenda zake mlimani kuomba. “**

- Ni ili upate nguvu za roho mtakatifu za kukusaidia ktk wokovu

**Luk 11:13**

**“Basi, ikiwa ninyi mlio waovu mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema, je! Baba aliye mbinguni hatazidi sana kuwapa Roho Mtakatifu hao wamwombao? “**

- Ili upate ulinzi wa mungu na ushindi dhidi ya dhambi

**Yoh 17.15**

**“Mimi siombi kwamba uwatoe katika ulimwengu; bali uwalinde na yule mwovu.”**

- Ili injili ya Yesu ipate kuenea na kuwafikia wenye dhambi ambao hawajawahi kuona uweza wa Mungu.

**Rum 10:1**

**“Ndugu zangu, nitakayo sana moyoni mwangu, na dua yangu nimwombayo Mungu, ni kwa ajili yao, ili waokolewe. “**

Kama wewe ulivyookoka omba wengine nao waokoke utapata mema

# 3. AINA ZA MAOMBI

Kuna aina tatu za maombi ya kupeleka mbele za Baba wa Mbinguni yaani Mungu muumbaji.Nazo ni ;

- Maombi ya mtu aliyeokoka binafsi

**Mathayo 7:7**

**"Ombeni, nanyi mtapewa; tafuteni, nanyi mtaona; bisheni, nanyi mtafunguliwa"**

Aina hii ya maombi ya mtu wa kimataifa uliyeokoka ni unapeleka mahitaji yako peke mbele za Mungu kwa kupiga goti na kuomba mbele za Baba Mfano unataka tabia ya unyenyekevu iumbike ndani yako nawe huna hiyo basi unaamua kuomwomba Baba wa mbinguni unyenyekevu au umepungukiwa na hekima omba kwa Mungu naye atakupa au umepungukiwa na ridhiki mwombe wa mbinguni naye atakupa. Maombi binafsi unaomba peke yako humshirikishi mwenzako aliyeokoka au kanisa ukisaidiwa na Roho mtakatifu aliye ndani yako.

- Maombi ya Famili ya watu waliokoka.

Aina hii ya maombi ya familia ya mtu wa kimaitaifa uliyeokoka unapaswa kuomba na familia yako kila siku nyumbani ili kupeleka mbele mungu mahitaji ya familia yako.Kama Baba lazima ukae chini wewe,mkeo na watoto uwaeleze maono/malengo uliyo nayo juu familia yako na wao pia wachangie wanataka kielimu,kiuchumi au kiushirika na mungu  familia iweje baada ya muda Fulani.Kisha kama familia mnatenga muda wa kuombea maono/malengo ya familia.

- Maombi ya pamoja ya waliokoka (kanisa)

Aina hii ya maombi ya kanisa ni kuombea maono ya huduma/kanisa,viongozi/watumishi wa kanisa kama wachungaji na maaskofu.

# 4. JINSI YA KUOMBA

Ukweli mtu wa kimataifa uliyeokoka unaye msaidizi ndani roho mtakatifu huyo ndiye anaweza kukuombea mbele za Baba wa mbinguni Je waamini? Unapotaka kuomba nenda mbele za mungu fumbua kinywa na useme mahitaji yako naye atakupa maneno ya kusema Baba wa mbinguni.

**Rum 8:26 - 27**

**"Kadhalika Roho naye hutusaidia udhaifu wetu, kwa maana hatujui kuomba jinsi itupasavyo, lakini Roho mwenyewe hutuombea kwa kuugua kusikoweza kutamkwa.**

**Na yeye aichunguzaye mioyo aijua nia ya Roho ilivyo, kwa kuwa huwaombea watakatifu kama apendavyo Mungu."**

Ukiomba mbele za Mungu zingatia mambo yafuatayo na Baba wa mbinguni atakusikiliza na kukujibu ukiomba kwa Imani ya Yesu:

- Omba rehema/msamaha/tubu juu makosa/dhambi/uovu unaoufahamu weka mikakati ya kuicha.Rehema kwa uovu / dhambi usiyoifahamu/unaoufahamu.
- Msifie kwa maneno yako ili kushusha au kukaribisha uwepo wake/ nguvu zake au Roho mtakatifu.Sema maneno ya sifa au mwimbie mungu tenzi au zaburi. Zaburi ni kitabu kipo ktk biblia na tenzi kitabu kinachouzwa na maduka ya vitabu ya wakristu unaweza kukinua unaweza kukipata kama mtumiaji wa kompyuta bure ktk tovuti ya www.mhubiriwakimaifa.org

**Waef 5:18-19**

"**...bali mjazwe Roho;mkisemezana kwa zaburi na tenzi na nyimbo za rohoni, huku mkiimba na kumshangilia Bwana mioyoni mwenu;"**

- Mshurukuru Mungu kwa Matendo mema aliyokutendea katika

# 5. JINSI YA KUOMBA

Wokovu wako yaani maisha mapya ndani ya Yesu. Matendo mema Yesu hukutendea kama Muujiza kuokoka, uponyaji,Kutolewa pepo au nguvu za giza,Miujiza,Baraka,Utajiri,uzima n.k

- Omba mahitaji yako mbele Baba wa Mbinguni au Mungu muumbaji aliyeumba dunia na vyote vinavyoonekana.
- Maombi yazingatie neno la Mungu au maandiko matakatifu. Ombi lako ambatanisha na kile alichosema Yesu ktk Biblia. Jifunze kuambatanisha ombi lako na maandiko matakatifu yalimo hasa injili za Mathayo,Marko,Yohane Na Luka na kuyasimamia maana ndiyo kweli. Mfano wa kuomba Roho mtakatifu unasema Mungu naomba nijaze roho mtakatifu Yesu amesema ktk **Luk 11: 13** tuombe roho mtakatifu Mungu utatupa. **"Basi, ikiwa ninyi mlio waovu mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema, je! Baba aliye mbinguni hatazidi sana kuwapa Roho Mtakatifu hao wamwombao?"** Kwa sababu hiyo uwe unapenda kusoma na kutafakari Biblia kwa bidii huku ukishirikisha Roho mtakatifu akufundishe ya Yesu yaliyomo ktk maandiko matakatifu ya biblia.
- Ktk kuomba kwako ikiwa hitaji lako unalompelekea Baba wa mbinguni kwa njia Yesu aliwahi kukutendea jifunze kumbusha kuwa anaweza aliwahi kukutendea, Mfano kama uliomba baraka ktk biashara au kampuni yako akakupa sasa umefungua nyingine mwombe na umkumbushe alivyokubariki naye atakutendea au ulikuwa ugonjwa tumbo ulimwomba Yesu akakuponya leo unaumwa malaria mwombe akuponye malaria kwa kumkumbusha uweza wake Yesu kuwa aliwahi kukuponya tumbo hawezi kushindwa malaria.
- Mshukuru Baba wa Mbinguni Mungu kwa kusikiliza maombi yako

# 6. MAOMBI YALIYO MAPENZI YA MUNGU

Maombi yaliyo mapenzi ya mungu ni yale unayoomba sawa na ulivyokusudiwa na mungu  baada ya kufunuliwa na Roho mtakatifu au sawa na Yesu au Baba wa mbinguni alivyosem alivyosema au maandiko yamesavyo.

Mahitaji unaweza kuomba mbele za Baba wa mbinguni na ni mapenzi yake ni yafuatayo:

- Omba mungu akujaze Roho mtakatifu kiasi cha kipimo cha Yesu sawa na uwezo wa moyo wako kubeba nguvu za mungu aliokuumba nao siku ulipookoka au sawa na alivyokukusudia. **Luk 11: 13 "Basi, ikiwa ninyi mlio waovu mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema, je! Baba aliye mbinguni hatazidi sana kuwapa Roho Mtakatifu hao wamwombao?**
- Omba utajiri 1wafalme 3:11 **Mungu akamwambia, Kwa kuwa umeomba neno hili, wala hukujitakia maisha ya siku nyingi; wala hukutaka utajiri kwa nafsi yako; wala hukutaka roho za adui zako; bali umejitakia akili za kujua kuhukumu;**
- Omba hekima ya Yesu kama Baba uliyeokoka na una familia unataka kuiongoza ktk mpango wa mungu au ni kiongozi wa kanisa la waliookoka mfano mwalimu, mchungaji, askofu, shemasi. mtume, nabii, mwinjilisti,Mhubiri umewekwa juu ya watu wa mungu waliokoka.**Yakobo 1:5  "Lakini mtu wa kwenu akipungukiwa na hekima, na aombe dua kwa Mungu, awapaye wote, kwa ukarimu, wala hakemei; naye atapewa." 1 Wafalme 3:12" basi, tazama, nimefanya kama ulivyosema. Tazama, nimekupa moyo wa hekima na wa akili; hata kabla yako hapakuwa na mtu kama wewe, wala baada yako hatainuka mtu kama wewe. "**

## 7. MAOMBI YALIYO MAPENZI YA MUNGU

- Omba maisha ya siku nyingi aliyoamuru mungu ni miaka 120. Ni mapenzi ya mungu wewe uishi na kuifikia hiyo miaka.
- **"1wafalme 3:11 Mungu akamwambia, Kwa kuwa umeomba neno hili, wala hukujitakia maisha ya siku nyingi; wala hukutaka utajiri kwa nafsi yako; wala hukutaka roho za adui zako; bali umejitakia akili za kujua kuhukumu"**
- **"Mwanzo 6:3 Bwana akasema, Roho yangu haitashindana na mwanadamu milele, kwa kuwa yeye naye ni nyama; basi siku zake zitakuwa miaka mia na ishirini. "**
- Omba mahitaji yako yaliyo mema ndio mapezi ya Mungu utapata kinyume chake hupati.
- **"Yakobo 4:3 Hata mwaomba, wala hampati kwa sababu mwaomba vibaya, ili mvitumie kwa tamaa zenu."**
- **"Mathayo 7.9—11 Au kuna mtu yupi kwenu, ambaye, mwanawe akimwomba mkate, atampa jiwe? Au akiomba samaki, atampa nyoka? Basi ikiwa ninyi, mlio waovu, mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema, je! Si zaidi sana Baba yenu aliye mbinguni atawapa mema wao wamwombao?"**
- Omba maji yaliyo hai hutaona kiu ya haki tena kiu yako itatiishwa,
- **"Yoh 4.10 Yesu akajibu, akamwambia, Kama ungaliijua karama ya Mungu, naye ni nani akuambiaye, Nipe maji ninywe, ungalimwomba yeye, naye angalikupa maji yaliyo hai."**
- **"Yoh 7:38 - 39 Aniaminiye mimi, kama vile maandiko yalivyonena, mito ya maji yaliyo hai itatoka ndani yake. Na neno hilo alilisema katika habari ya Roho, ambaye wale wamwaminio watampokea baadaye; kwa maana Roho alikuwa hajaja, kwa sababu Yesu alikuwa hajatukuzwa."** Maji yaliyo hai ni roho mtakatifu aliye ndani yako uliyeokoka au Upako kwa watumishi

## 8. MAMBO YA KUZINGATIA KABLA YA KUOMBA

- Msamaha — Kabla kuomba unatakiwa usiwe na uchungu moyoni kama kuna mtu amekukosea unatakiwa kumsamehe. Msipomsamehe nawe hutasamehewa unaingia kuomba rehema au msamaha mungu naye hakusamehe hivyo hatajibu maombi yako.“**Marko 11:25 Nanyi, kila msimamapo na kusali, sameheni, mkiwa na neno juu ya mtu; ili na Baba yenu aliye mbinguni awasamehe na ninyi makosa yenu. “**
- Kujichunguza na kutafakari njia zako kama makosa umefanya upate kuyatubu au hujatii sauti ya mungu au agizo lake upate kuyatubu.
- Mapatano — Heshimu mapatano na yule aliyeokoka unayeomba naye au kanisa. Ukimshirikisha jambo lolote jema la kuombea mkapatana kuomba siku 3 kwa kufunga ikiwa mmoja atavunja mapatano ni kosa unapaswa kurudia.Hata kama mungu angejibu maombi yenu siku ya pili unapaswa kumalizia kuomba na kufunga siku ya tatu kumbuka mungu ni kweli jifunze kuwa kama yeye.Ikitokea mwenzako akashindwa kufunga mfano siku ya 3 bila sababu ya msingi Mungu anaweza asiwajibu.Kumbuka maombi ya mapatano hujibiwa haraka kwa sababu umoja mungu hupenda umoja yaani akiwaona watu wake wakishirikiana pamoja kama yeye na Yesu ni wamoja.“**Mathayo 18.19 Tena nawaambia, ya kwamba wawili wenu watakapopatana duniani katika jambo lo lote watakaloliomba, watafanyiwa na Baba yangu aliye mbinguni. “**
- Imani — Jichunguze kabla ya kuomba je yale unayoomba unaamini Yesu anaweza kukutendea kama una mashaka usiombe maana hutapata.”**Yakobo 1:6—7 Ila na aombe kwa imani .. Maana mtu kama yule asidhani ya kuwa atapokea kitu ..“**

## 9. JINSI YA KUFAHAMU MAJIBU YA MAOMBI YAKO

Ukitaka jinsi ya kufahamu majibu ya maombi yako fuata utaratibu ufuatao utakufanya ufahamu Yesu yu ndani yako au lako.

- Andika mahitaji yako au haja ya moyo wako kwenye daftari yako (Notebook), Notebook yako ya simu au Computer document yale unataka kuomba au unayoomba mbele za mungu.
- Kabla ya kuomba kila siku pitia notebook yako angalia yale uliyoomba kama yamejibiwa weka alama tick kwa yaliyojibiwa kwa siyojibiwa usiweke alama mpaka yajibiwe ndiwe utick.
- Mshukuru mungu kwa yale yaliyojibiwa kwa kumwambia mungu asante ktk maombi nenda kashudie kanisani na kwa watu wa kimaitaifa pia waliokoka na wasiookoka, ndugu zako,jamaa zako,wafanyakazi wenzako,rafiki zako au jirani zako.

Hivyo ndivyo jinsi ya kutambua yale unayoomba yanajibiwa ushirika wako na mungu kwa njia ya maombi uko vizuri au kuna shida. Mfano wa mtu aliyeomba akajibiwa ktk biblia

**Luk 2:36 — 38 Palikuwa na nabii mke, jina lake Ana, binti Fanueli, wa kabila ya Asheri, na umri wake ulikuwa miaka mingi, alikuwa amekaa na mume miaka saba baada ya uanawali wake. Naye ni mjane wa miaka themanini na minne; haondoki katika hekalu, ila huabudu usiku na mchana kwa kufunga na kuomba. Huyu alitokea saa ile ile akamshukuru Mungu, na wote waliokuwa wakiutarajia ukombozi katika Yerusalemu akawatolea habari zake. “** Pia mfano mwingine unaweza kusoma ktk biblia kitabu cha **1samwel 1**

# 10. NANI AOMBE?

Ee mtu wa kimataifa uliyeokoka unapaswa kufahamu nani anastaili au wana haki kama ya kuomba mbele za Baba wa Mbinguni na kujabiwa:

- Watu waliookoka wampendao Baba wa mbinguni

**"1 Wathesalonike 5:17 ombeni bila kukoma;"** Mtume Paulo analigiza kanisa (wtu wliokoka)agizo la Yesu la kudumu ktk maombi

- Mitume/Watumishi waliotumwa na Yesu wakubwa **Yoh 14. Yesu alikuwa asema na mitume jinsi mambo kadhaa majawapo ni maombi wakimwomba Baba yake lolote jema hilo Yesu atalifanya.**
- Wanafunzi wa Yesu

Wanafunzi wa Yesu kwa wakati huu ni waliokoka na waokaa chini ya fundisho la mitume au watumishi waliotumwa na Yesu na kufundishwa naye au kwa roho wake mtakatifu kama waalimu wa kanisala waliokoka wale wakubwa. Wanafunzi wa Yesu wanapatikana ubatizo wa toba wa maji mengi kama wa Yesu Yordani tunataraji nao kujaa roho mtakatifu baada huo ubatizo kama Yesu ni sawa na kuokoka

**" Math 28:19 Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu;**

**28.20 na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari.**

**"Luk 11:1 Ikawa alipokuwa mahali fulani akiomba, alipokwisha, mmoja katika wanafunzi wake alimwambia, Bwana, tufundishe sisi kusali, kama vile Yohana alivyowafundisha wanafunzi wake. "**

**"Marko 11:24 Kwa sababu hiyo nawaambia, Yo yote myaombayo mkisali, aminini ya kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu. "**

**Zingatia** :Kwa upande wa wenye dhambi yaani wasiokoka ni sala ya toba tu peke yake ndio husikilizwa mbele za mungu na kujibiwa ikiwa ataacha kabisa ile dhambi aliyotubiwa.

# 11.SHUKRANI

Ee mtu wa kimaifa uliyeokoka shukrani ni muhimu kwa mungu. Mtoto ambaye akimwomba baba yake kitu anachohitaji kama uniform ya shule akinunuliwa na babaye kisha kumwambia babaye asante siku nyingine akipata uhitaji mwingine akaenda kwa babaye na kuomba hupewa kwa wakati acheleweshewi tofauti na yule asiyesema asante.yaani asiyeshukuru akitendewa mema.

Ee mtu wa kimaifa uliyeokoka uwe mwenye moyo wa shukrani kwa Baba wa mbinguni ajibupo maombi yako kwa maneno ya kinywa chako mfano kwa kushukuru na kushudihudia yale Baba wa mbinguni aliyokutendea baada ya kumwomba haja ya moyo wako au kwa utoaji sadaka ya shukrani kwa kanisa la waliokoka.

**2 Wakor 1:11 ninyi nanyi mkisaidiana nasi kwa ajili yetu katika kuomba, ili, kwa sababu ya ile karama tupewayo sisi kwa msaada wa watu wengi, watu wengi watoe shukrani kwa ajili yetu.**

Ukiomba gari au nyumba Baba wa mbinguni akikupa Kimiujiza usisahau kushukuru au kumwambia asante Yesu na Baba yako kwa kunipendelea .

**"Walawi 7:12 Kwamba aitoa kwa ajili ya shukrani, ndipo atakaposongeza pamoja na hiyo sadaka ya shukrani mikate isiyotiwa chachu, iliyoandaliwa na mafuta, na mikate ya kaki isiyochachwa iliyopakwa mafuta, na mikate ya unga mwembamba uliolowama mafuta."**

Mshukuru Baba wa mbinguni kwa mapato ya kazi ya mikono yako kwa yale anakutendea unapoombaji mahitaji yako mbele za mungu yaani mshukuru mungu kwa matoleo mfano Pesa/fedha ya ujira wa kazi ya mikono, kondoo au ng'ombe unapata kwa mwaka kutoka na mifugo yako unayofuga.Mshukuru Baba wa mbingguni kwa mikate na divai inayotokana na ngano na zabibu unazolima. Ktk maandiko matakatifu ya Walawi 7:12 inazungumzia kutoa shukrani mbele za mungu kwa njia ya utoaji ya kile unachopata ktk kazi za mikono.

## 12. SALA NI NINI?

Sala ni maombi ya kila siku yenye mahitaji yale yasiyobadilika na maneno pia.Ipo sala moja tu Yesu aliwafundisha wanafunzi wake kusali.Soma ktk maandiko matakatifu ya biblia

**Mathayo 6:9 - 14**

**“Basi ninyi salini hivi; Baba yetu uliye mbinguni, Jina lako litukuzwe, Ufalme wako uje, Mapenzi yako yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni. Utupe leo riziki yetu. Utusamehe deni zetu, kama sisi nasi tuwasamehevyo wadeni wetu. Na usitutie majaribuni, lakini utuokoe na yule mwovu. [Kwa kuwa ufalme ni wako, na nguvu, na utukufu, hata milele. Amina.] Kwa maana mkiwasamehe “**

Mahali pa kusali ni hekaluni au ktk nyumba ya mungu ukitaka kusali sala kama hiyo kwenda hekaluni au ktk nyumba ya mungu ni muhimu kama huna nyumba na chumba cha ndani ya nyumba cha sala.Pengine unaishi nyumba ya kupanga,apartment au chumba cha kuomba panga sala kama hiyo hapo juu hairusiwi kusali.

**Mathayo 21:12 — 13**

**“Yesu akaingia ndani ya hekalu, akawafukuza wote waliokuwa wakiuza na kununua hekaluni, akazipindua meza za wabadili fedha, na viti vyao waliokuwa wakiuza njiwa;**

**akawaambia, Imeandikwa, Nyumba yangu itaitwa nyumba ya sala; bali ninyi mmeifanya kuwa pango la wanyang'anyi. “**

Mahali pa kusali ni ktk chumba cha ndani ya nyumba yako tunasoma ktk maandiko yafuatayo:

**Mathayo 6.6**

**“Bali wewe usalipo, ingia katika chumba chako cha ndani, na ukiisha kufunga mlango wako, usali mbele za Baba yako aliye sirini; na Baba yako aonaye sirini atakujazi. “**

**NB: “Math 21.22 Na yo yote mtakayoyaomba katika sala mkiamini,”**

## 13. TOFAUTI YA SALA NA MAOMBI

- **Sala** ni maombi ya kila siku yenye mahitaji yale yasiyobadilika na maneno pia.Ipo sala moja tu Yesu aliwafundisha wanafunzi wake kusali.Soma ktk maandiko matakatifu ya biblia Wakati **Maombi** ni njia ya kumueleza Mungu haja/mahitaji ya moyo wako. Mahitaji ni yale yaliyoshindikana kwako sio kwa mwingine.Haja au mahitaji ya moyo wako hufamika kama kiu ya moyo wako.Mfano; kiu ya kumwona mungu,haja kuona nguvu za kazi ktk utumishi wake,mahitaji ya moyo wake ya chakula, malazi,pesa,mavazi,watoto, utajiri,Gari n.k
- **Sala** haibadiliki ipo moja iliyofundishwa na Yesu ktk **Mathayo 6 : 9 - 14** wakati **Maombi** ni mapya kila siku kutegemea haja za moyo zinazoibuka kila wakati
- **Sala** hufanyika ktk chumba cha ndani ya nyumba yako au hekaluni yaani nyumba ya mungu wakati **maombi** hufanyika hekaluni **1samweli 1** hata nje ya nyumba yako na hekalu mfano kwenye milima "**Luk 9:28 Baada ya maneno hayo yapata siku nane, aliwatwaa Petro na Yohana na Yakobo, akapanda mlimani ili kuomba. "**
- **NB :** Hekalu ni nyumba ya mungu iliyotumika kwa maombi na ibada tangu agano la kale hufanania na jingo la kanisa yanayojengwa sasa.Ukweli kulingana kitabu cha **matendo ya mitume 2,2:46**
- kuna kasoro ktk ujenzi wa majengo ya kanisa ukweli majengo ya kanisa yalipaswa yajengwe kama hekalu na maelezo yapo ktk kitabu cha nabii **Ezekiel 40:1** kwa sababu yule alitumwa kuanzisha kanisa ambaye ni mtume Petro alikaa na kanisa(Waliokoka) hekaluni.

## 14. ROHO MTAKAKATIFU

Roho mtakatifu mtu wa kimataifa uliyeokoka aliye ndani kama msaidizi ktk maisha yako ya wokovu hukusaidia pia ktk kuomba Yesu hakusema msaada wa maombi wa kutoka kwa roho mtakatifu lakini mhubiri,mwalimu na mtume Paulo wa mataifa asema ktk biblia kitabu cha **Rum 8:26 –27** juu ya msaada wa roho mtakatifu tunapoomba mahitaji yetu mbele Baba wa mbinguni.

**"Kadhalika Roho naye hutusaidia udhaifu wetu, kwa maana hatujui kuomba jinsi itupasavyo, lakini Roho mwenyewe hutuombea kwa kuugua kusikoweza kutamkwa.**

**Na yeye aichunguzaye mioyo aijua nia ya Roho ilivyo, kwa kuwa huwaombea watakatifu kama apendavyo Mungu. "**

Ee mtu wa kimaitaifa uliyeokoka usishangae ile hali ya kutoweza kuomba kwa siku za mwanzo za kuokoka kadri unavyoshiriki ktk maombi ya ushirika ya kanisa na kusoma biblia kuna kukua ktk kuomba kwa msaada wa roho mtakatifu. Kipindi hicho cha mwanzo wa safari yako ya kujifunza kuomba mbele za mungu roho mtakatifu hutuombea mbele za Baba wa mbinguni mahitaji yetu.

**Yoh 14.26**

**"Lakini huyo Msaidizi, huyo Roho Mtakatifu, ambaye Baba atampeleka kwa jina langu, <u>atawafundisha yote,</u> na kuwakumbusha yote niliyowaambia. '**

Ukimwomba akufundishe kuomba kama apendavyo Yesu atakufundisha yote juu ya kuomba uliyosema Mungu ktk biblia sawa na sehemu yako uliyotakiwa kujulishwa siri ya kuomba ktk ufalme wa mungu mbele za Baba wa mbinguni hata ukapata.

Ukiomba huyo msaidizi akufundishe juu ya kusimamia maandiko matakatifu ya biblia  na kuambatanisha na haja za moyo unazoomba mbele za mungu yaani Baba yake Yesu atakufundisha.

## 13. NENO LA YESU

**Yoh 15.7**

**"Ninyi mkikaa ndani yangu, na maneno yangu yakikaa ndani yenu, ombeni mtakalo lote nanyi mtatendewa. "**

Ninyi mkikaa ndani yangu maana yake ni kuokoka kama umeokoka ee mtu wa mtu wa kimataifa upo ndani ya Yesu la bado kaookoke na Maneno yangu kukaa ndani yenu ni kuyatafakari,kuyakumbuka na kuyaweka ktk matendo ili upate mabadiliko ya kimaisha na kitabia yaliyo ya mungu na mungu akakufurahia ndipo omba lolote jema na Baba wa mbinguni atakupa kwa wakati.

Mwenye kutendea kazi neno la Yesu au injili yake huyo amemfanya mungu kuwa mkweli au amemshuhudia mungu kuwa ni kweli ktk maisha yake.

**Yoh 16.23—24**

**"Tena siku ile hamtaniuliza neno lo lote. Amin, amin, nawaambia, Mkimwomba Baba neno lo lote atawapa kwa jina langu. Hata sasa hamkuomba neno kwa jina langu; ombeni, nanyi mtapata; furaha yenu iwe timilifu. "**

Ni neno la Yesu la ahadi kwa waombao kwa jina lake mbele za Baba wa mbinguni atawapa. Omba mambo mema ambayo akikupa utapata furaha ktk maisha yako mapya ya ufufuko wa yesu (wokovu) na kumtukuza Mungu baba yake Yesu.

**Mathayo 26.41**

**"Kesheni, mwombe, msije mkaingia majaribuni; roho i radhi, lakini mwili ni dhaifu."**

Ni neno la Yesu lenye agizo la kukesha.kulitii na kupata mbaraka wake penda kushirikiana wenzako waliokoka ktk kanisa ktk mikesha ya maombi inayopangwa na kanisa la waliokoka. Ee mtu wa kimataifa uliyeokoka ujifunze kuitakari hiyo mikesha na faida unayopata kwa kudhuhuria ktk wokovu wako.

## 15. KUOKOKA

Kama hujaokoka ewe mtu wa kimataifa na unataka kuokoka kiri maneno yafuatayo kwa kinywa chako kwa Imani Sema,

"Bwana yesu ninakuja kwako mimi ni mwenye dhambi natubu naamini ya kwamba ulisulubiwa kwa ajili ya dhambi zangu na laana zake damu yako ilimwagika nipate ondoleo la dhambi na kupatanishwa na baba yako na ulipigwa nipate ondolewa dhambi zangu, nisamehe dhambi zangu na uniondolee bila kusahau laana zake na ulifufuka nipewe maisha mapya huru mbali na dhambi na laana zake yaani maisha ya haki na baraka Yesu ingia ktk maisha yangu na ufalme wa mungu pamoja na roho mtakatifu unipe maisha hayo ya haki yako na baraka zake pia.Andika jina langu mbinguni nijaze furaha yako ya kunisamehe na kuniondolea dhambi na laana yake na kufanyika mwana mbinguni na kupewa sehemu ya urithi wako wa kutembea na nguvu na mamlaka ya mungu wako ya kuzivunja na kuziharibu kazi za shetani ikiwepo mapepo,magonjwa n.k. Asante yesu kwa kuniokoa , kwa roho mtakatifu, kwa neema yako, kwa karama au vipawa vyako, mamlaka yako, ufalme wako na nuru yako maana umeyafanya maisha yangu kuwa na uzima wako ... Amen"

Sasa umeokoka tafuta kanisa au huduma ya waliokoka na ushirikiane nao ili upate kukua hata kufikia ufahamu wa cheo cha kristo yaliyo ktk nchi yako au bara lako lakini kama upo Tanzania karibu efatha church yapo makanisa au huduma zingine za waliokoka au Ben Hinny ministry kama upo Marekani ; Paula white ministry n.k Yesu akuongoze kwa Roho wake mtakatifu kukupeleka ktk kanisa au huduma ya waliokoka ambayo utakuwa kufikia ufahamu wa cheo cha kristo ili Yesu akutumie sawa na kusudi lake la kukuokoa.

## 16. MWISHO

Kitabu cha kuokoka kwa **mtu wa kimataifa** kipo kukupa ufahamu wa yesu uliyempokea alichokutendea yeye na Baba yake wa mbinguni mpende kwa kulitii neno lake mfano **mafundisho yake** na **nabii zake .**

Ukitaka kuwasiliana na Mtumishi ya Yesu Mhubiri wa kimataifa Lameck Lister :


**Tovuti:** www.mhubiriwakimaifa.org

**Baruapepe:** listlameck5@gmail.com

**Simu:** +2550658601034 or 0658601034

**Sanduku la Barua:** Efatha Church: P.o Box 35666

Mwenge DSM Tanzania



Mhubiri wa kimataifa Lameck Lister niliokoka mwaka 2003 kwa kuongozwa sala ya kuokoka na Paul Roberty nilipokuwa kidato cha Tatu Kibaha Sekondari nikiwa na umri wa miaka 17 ndipo nilipoupokea ufalme wa mungu.

**Mafundisho ya kukulia wokovu na Ubatizo wa maji mengi**

Mafundisho ya kukulia wokovu na ubatizo niliyapata ktk kanisa la Efatha mwaka 2003-2006. Yanahusu maisha mapya ya mtu aliyeokoka anavyotakiwa kuishi na ubatizo wa kristo. Ndani ya hayo mafundisho yanazungumzia maisha ya toba. tofauti ya maisha kabla hujaokoka na baada ya kuokoka na kile Yesu na baba yake amefanya ndani ya mtu aliyeokoka.

**Mafundisho ya Roho mtakatifu**

Mafundisho ya roho mtakatifu niliyapata mwaka 2007 ktk kanisa la Efatha - Mwenge DSM Tanzania. Na kuwekewa mkono na Mtume na Nabii Josephat . E. Mwingira mkuu na mwanzilishi wa kanisa la Efatha ili kujaa roho mtakatifu kwa upya na vipawa au karama kama ilivyo neema ya Mitume itokayo kwa Yesu kristo.

**Utumishi wa mungu**

Baada ya kumaliza mafundisho yote nimepewa cheti cha utumishi wa mungu cha ufahamu wa cheo cha kristo. Natambulikana ndani ya kanisa la Efatha kama Mtumishishi wa mungu mbele baba yake Yesu na Yesu kama mhubiri wa kimataifa. Ukitaka kuona cheti cha utumishi wa mungu nilichopata Ktk Kanisa la Efatha

Website:www.mhubiriwakimataifa.com

Email:listlameck5@gmail.com

Mobile: +255658601034 ; 0658601034